**HOTUBA YA IJUMAA**

**Haki ya kupigania nchi**

**Imefasiriwa**

**na**

**profesa Ayman Alasar**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe, msemaji ndani ya Kitabu chake Kitakatifu: **وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا** {**Shikamaneni nyote na njia ya Mwenyezi Mungu wala msitafautiane**}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki ya kuabudiwa isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma na amani pamoja na baraka kwake na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wote wenye kuwafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya Utangulizi**:

Nchi ni sehemu yenye thamani kubwa ndani ya nyoyo za wananchi wake, na kuwa na hali ya uzalendo ni maumbile ya nafsi ya mwanadamu, kwani anasema Al-Aswmai R.A: Pindi unapotaka kufahamu kujua uaminifu wa mtu na uamifu wa ahadi yake basi angalia upendo wake kwa nchi yake na upendo wake kwa ndugu zake na kuujutia wakati wake uliopita.

Kupenda nchi na uzalendo kwa nchi ni jambo la lazima kidini, hivyo Sharia ya Kiislamu imetoa wito wa kuwa na uzalendo na nchi pamoja na kufanya kazi kwa ajili ya ustawi wake na maendeleo, huyu hapa Mtume wetu Muhammad S.A.W pindi alipohama Makka na kuhamia Madina aliangalia mji wake wa Makka akiwa anauaga na akasema: “Ni mji mzuri ulioje! Ninakupenda sana! Lau watu wangu wasingenitoa kwako basi nisingetoka”. Na pindi alipofika Madina na kuanza maisha alimuomba Mwenyezi Mungu kumjaalia upendo kwa mji wa Madina, akasema Mtume S.A.W: Ewe Mwenyezi Mungu tupe upendo kwa mji wa madina kama ulivyotupa upendo kwa mji wa Makka.

Jambo la kupenda nchi si kwa maneno tu au kuinua alama mbalimbali bali kupenda nchi ni kujitoa muhanga kwa kila kilicho na thamani, uzalendo wa kweli maana yake ni ufuasi nzuri na kupenda nchi pamoja na kuwa na shime kwa ajili ya amani ya nchi utulivu maendeleo na ustawi wake, kama vile una maanisha kuwajibika kikamilifu kwenye haki na wajibu, kwani uzalendo wa kweli ni uaminifu na kujifaharisha na nchi, kwa sababu nchi inahitaji kujitoa kwetu kwa lengo la kuipa nguvu na kuuinua pamoja na kuilinda.

Miongoni mwa haki muhimu kwa nchi ni kupigania, hakuna shaka kuwa kujio kwa nafsi ni katika aina bora ya kujitoa ambapo Anasema Mola Mtukufu:

**مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُم مَّن قَضَى نَحْبَهُ وَمِنْهُم مَّن يَنتَظِرُ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا**

{**Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwishakufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo**} na Mtume S.A.W ametoa bishara njema kwa walinzi wa nchi ambao wanajitoa kwa nafsi zao ikiwa ni kujikinga na adhabu ya motos, ambapo anasema Mtume SAW:

**عَيْنَانِ لَا تَمَسُّهُمَا النَّارُ، عَيْنٌ بَكَتْ مِنْ خَشْيَةِ اللهِ، وَعَيْنٌ بَاتَتْ تَحْرُسُ فِي سَبِيلِ الله.**

"*Macho mawili hayataguswa na moto, jicho limelia kwa ajili ya kumuogopa Mwenyezi Mungu, na jicho limekesha kulinda njia ya Mwenyezi Mungu*". Hivyo basi watu hawa wa kujitoa muhanga wanastahiki kuwa ni wateule wa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waumini, na kuwa pamoja na Mitume na walisadiki na wale waja wema, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَيَتَّخِذَ مِنكُمْ شُهَدَاءَ.**

{**Ili Mwenyezi Mungu awapambanue walio amini na awateuwe miongoni mwenu mashahidi**} na Anasema tena Mola Mtukufu:

وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِم مِّنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا.

{**Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wapamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao**}.

********

**HOTUBA YA PILI.**

Namshukuru Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimwendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume Muhammad S.A.W pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswhaba zake wote.

Miongoni mwa wajibu wa wananchi kwa nchi yao ni pamoja na kutoka wakiwa wepesi na wakiwa wazito ambapo maslahi ya nchi yanapeleka hivyo na ikiwa ni katika wajibu wao kujitoa fidia roho zao na damu zao wakati wowote hali ikihitaji hivyo, basi kushiriki kwao vizuri katika kila kinachopelekea masilai ya nchi ni katika uzalendo wa nchi na kupenda nchi na kuwa na nia safi na nchi.

Kwani garama ya nchi hailipwi na kizazi kimoja tu wala kulipwa na baadhi yao pasiya wengine, bali ni hali shirikikishi kwa vizazi vyote na vinavyofuata.

Miongoni mwa haki muhimu za nchi ni: Kuleta juhudi kufanya kazi na ustadi wa mambo, kwani Mtume S.A.W anasema: **إِنّ اللَّهَ يُحِبُّ إِذَا عَمِلَ أَحَدُكُمْ عَمَلًا أَنْ يُتْقِنَهُ** "*Hakika Mwenyezi Mungu anapenda mmoja wenu anapofanya kazi afanya kwa ustadi mkubwa*".

Na miongoni pia mwa haki: Kutekeleza wajibu wa kikazi, kwani utumishi ni amana na jukumu, na kutekeleza haki yake ni wajibu wa Kisharia na kitaifa, ama kupuuza kutekeleza wajibu wa kikazi ni katika aina hatari sana ya uharibifu, hivyo inapaswa

kwa kila mtu moyo wake na dhamira yake kuwa hai na macho pamoja na kuhisi siku zote kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنتُمْ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ.**

{**Naye yupamoja nanyi popote mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona mnayo yatenda**}.

Miongoni pia mwa haki: Ni kuheshimu bendera yake na wimbo wake wa taifa pamoja alama zengine za taifa, kwani benderea ni alama ya nchi na anuwani yake ambayo huzungukwa pembezoni mwake na wananchi wake wote waliomo ndani ya nchi na nje ya nchi, na wanafikia chini ya jina la nchi mafanikio yao, na kuheshimu pia vipaombele na misingi thabiti ya ujenzi wa nchi.

Pia miongoni mwa haki: Ni uwakilishi mzuri ndani ya nchi na nje ya nchi na katika majukwaa yote ya kitaifa na kimataifa, pamoja na shime ya kuinua bendera ya nchi katika nchi zote, na mtu kuwa balozi bora kwa nchi yake popote pale alipo.

Pia katika haki: NI kutoruhusu kuguswa kwa ardhi yake na mali zake na kupambana na maadui wa nchi ili kulinda tamko la nchi nafsi na mali wakati wowote litakapotakiwa hilo.

**Ewe Mwenyezi Mungu ilinde nchi yetu ya Misri pamoja na nchi zengine za ulimwengu wa Kiislamu na Kiarabu**.